

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA PILI**

**KIKAO CHA NNE**

**05 FEBRUARI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

KIKAO CHA NNE – TAREHE 05 FEBRUARI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

42. **MHESHIMIWA ALMAS ATHUMANI MAIGE  
(TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Wananchi wa Jimbo la Tabora Kaskazini wamejitolea kujenga Vituo vya Afya katika Kata za Ilolangulu, Mabama, Shitage na Usagari:-

Je, Serikali ipo tayari kuanza kuchangia miradi hiyo.

**43. MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL KUNAMBI (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ni Halmashauri mpya iliyotoka Wilaya ya Kilombero:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaipa Mlimba hadhi ya kuwa Wilaya hasa ikizingatiwa umbali mrefu wa takriban Km 200 ambao Wananchi wanatembea kufuata huduma Makao Makuu ya Wilaya;
- (b) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa majengo ya Halmashauri na kuboresha miundombinu ya barabara.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**44. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-  
Je, ni lini ujenzi wa Wodi ya Wazazi utanza katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga.

**45. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON  
MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la Hospitali ambazo zinaendelea kutoza fedha Akina Mama wanaojifungua kwa njia ya kawaida.

**46. MHESHIMIWA MAIDA HAMAD ABDALLAH  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kupambana na ugonjwa wa Malaria, bado ugonjwa huo unaendelea kuwaathiri Wananchi wakiwemo Watoto:-

Je, Serikali inaweza kutuambia hatua zilizofikiwa za kutokomeza ugonjwa huo.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**47. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA  
(KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kumpata Mwekezaji katika Shamba la Chai la Kidabaga.

**48. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itawalipa Wakulima wa Tangawizi Mamba Myamba; Wilaya ya Same ambao walifungiwa na SIDO mashine zisizo na kiwango cha kuchakata Tangawizi.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**49. MHESHIMIWA HAMISI SHAABANI TALETALE (MOROGORO KUSINI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Bigwa – Kisasi itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mwaka 2020 – 2025 inavyoelekeza.

**50. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga (Km 151) utaanza kwa kuwa upembuzi yakinifu umekamilika.

**WIZARA YA KILIMO:**

**51. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uzalishaji wa zao la Pareto ambalo mahitaji yake Duniani ni makubwa.

**52. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kukarabati miundombinu ya Skimu za umwagiliaji za Mnazi – Kwemkwazu na Mng'aro – Kitivo ambazo zimeharibiwa kabisa na mvua.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **53. MHESHIMIWA DAUD PROTAS VENANT (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Jimbo la Igalula lina jumla ya Vijiji 58, ambapo Vijiji 12 vimepata umeme na Vijiji 46 bado havijapata umeme:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Vijiji 46 ambavyo havijapata umeme;
- (b) Je, gharama za kuunganisha umeme kwa kila Mwananchi ni kiasi gani.

### **54. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Ofisi ya TANESCO Wilaya ya Muleba inazidiwa na wingi wa wateja kutokana na miradi ya REA:-

Je, ni lini Wilaya hiyo itapewa hadhi ya Mkoa wa TANESCO ili iweze kutoa huduma kwa wakati.

## **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

### **55. MHESHIMIWA ZAINAB ATHUMAN KATIMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha baadhi ya Sheria kandamizi kwa Wanawake ili ziendane na wakati.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **56. MHESHIMIWA FREDRICK EDWARD LOWASSA (MONDULI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mradi wa maji wa BN 520 una ziada ya lita milioni 100 kwa mujibu wa wataalamu, na Mhe. Rais alikubali ombi la ziada hiyo kujumuishwa kwenye mradi:-

Je, ni lini utekelezaji wa ahadi hiyo utaanza.

### **57. MHESHIMIWA DEODATUS PHILLIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini mradi wa kusambaza maji Mji wa Njombe kutoka Mto Hagafilo utaanza.



### III. HOJA ZA SERIKALI:

#### WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa lijadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoitoa wakati wa Ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili tarehe 13 Novemba, 2020.

*(Majadiliano yanaendelea)*



DODOMA  
05 FEBRUARI, 2021

S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE